# UFUNUO (SEHEMU YA 11)

Matayo 16:13 – 20,……………………. Na Yesu alijibu, akamwambia Heri wewe Simoni Bar-yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili; bali Baba yangu aliye Mbinguni …….. (mstari wa 17).

Natusikilize zaidi kile Nabii wa Mungu alisema kuhusu "Ufunuo".

Umuhimu wa ufunuo wa Roho kwa mwaminio wa kweli hauwezi kamwe kutiliwa mkazo sana. Ufunuo unamaanisha mengi zaidi kwako labda kuliko unavyotambua. Sasa sizungumzii juu ya Kitabu hiki cha Ufunuo na kukuhusu wewe. Ninazungumza juu ya mafunuo YOTE. Ni muhimu sana kwa Kanisa. Je! Unakumbuka katika Mathayo 16 ambapo Yesu aliwauliza wanafunzi swali hili? "Watu hunena kwamba Mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?" Nao wakasema, "Wengine hunena u Yohana Mbatizaji: wengine, Eliya; na wengine Yeremia, ama mmojawapo wa manabii." Akawaambia, "Lakini ninyi mwaninena Mimi kuwa ni nani?" Ndipo Simoni Petro akajibu akamwambia, "Wewe Ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Naye yesu akajibu akamwambia, "Heri wewe, Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye Mbinguni. Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda " Wakatoliki wa Kiroma wanasema ya kwamba Kanisa limejengwa juu ya Petro. Sasa hicho ni kimwili kweli. Mungu angewezaje kulijenga Kanisa juu ya mtu anaeyumba hivi kwamba hata alimkana Bwana Yesu na akalaani alipokuwa anafanya hivyo? (Matayo 26:69-75) Mungu hawezi kulijenga Kanisa lake juu ya mtu aliyezaliwa katika dhambi. Wala haikuwa ni mwamba fulani uliokuwa umelala pale kana kwamba Mungu alikuwa ameitakasa ardhi ya mahali pale. Wala si kama vile Waprotestanti wanavyosema, ya kwamba Kanisa limejengwa juu ya Yesu. Ilikuwa ni UFUNUO. Lisome jinsi lilivyoandikwa: "Mwili na damu HAVIKUKUFUNULIA hili, BALI BABA YANGU NDIYE ALIYEKUFUNULIA, na JUU YA MWAMBA HUU (Ufunuo) nitalijenga kanisa langu:" (Matayo 16:17) Kanisa limejengwa juu ya Ufunuo, juu ya "Bwana Asema Hivi".

Habili alijuaje la kufanya kusudi amtolee Mungu dhabihu inayokubalika? (Mwanzo 4:3-8.) Kwa imani yeye alipokea ufunuo wa damu. Kaini hakupata ufunuo wa namna hiyo (hata ingawa alikuwa na agizo) kwa hiyo hangeweza kutoa dhabihu iliyo sahihi. Ilikuwa ni ufunuo kutoka kwa Mungu ulioleta tofauti na ukampa Habili uzima wa milele. Sasa ungeweza kuchukua yale mchungaji anayosema, ama yale yanayofundishwa na seminari na ingawa yanaweza kufundishwa kwako kwa ufasaha wa maneno, mpaka Mungu atakapokufunulia ya kwamba Yesu ndiye Kristo, na ya kwamba damu ndiyo inayokusafisha, na ya kwamba Mungu ndiye Mwokozi wako, hutapata uzima wa milele kamwe. Ni Ufunuo wa roho ndio unaotenda jambo hilo

Sasa nilisema ya kwamba Kitabu hiki cha Ufunuo ni ufunuo wa Yesu na yale anayofanya katika Makanisa katika hizo nyakati saba. Ni ufunuo kwa sababu wale wanafunzi wenyewe hawakujua kweli hizi zilizoandikwa. Haikuwa kwanza imefunuliwa kwao. Mnakumbuka ya kwamba walimjia Yesu katika Kitabu cha Matendo na kumwuliza, "Je! Wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme?" Naye akasema, "Si kazi yenu kujua nyakati wala majira." (Matendo 1:6 – 8) Watu hao walikuwa wangali wanamfikiria Yesu kuwa na ufalme waduniani. Lakini ilikuwa ufalme wa kiroho ambao Yeye alikuwa anaenda kujenga. Hata Yeye hakuweza kuwaambia kuhusu mahali pake katika huo, kwa maana Baba hakuwa amemfunulia. Lakini sasa baada ya kufa na kufufuka kwake, na kwa wakati huu maalum katika huduma yake ya upatanisho, Yeye anaweza kumwonyesha Yohana hapa katika ufunuo huu wa nafsi yake mwenyewe mambo yale ambayo utukufu na uwepo wake Kanisani yatamaanisha na kufanya.

Katika ufunuo huu yeye anatwambia mwisho wa ibilisi ni nini. Anatwambia jinsi atakavyomtenda ibilisi na kumtupa katika ziwa la moto. Anafunua mwisho wa watu waovu wanaomfuata shetani. Na Shetani anachukia jambo hilo (Ufunuo 20: 7-15).

Je! Umeshaona jinsi Shetani anavyochukia vitabu viwili vya Biblia zaidi kuliko vingine vyote? Kwa kuwatumia wanatheolojia wa kimapinduzi na wanasayansi bandia yeye daima hushambulia Kitabu cha Mwanzo na Kitabu cha Ufunuo. Katika vitabu hivi vyote viwili tunaona mwanzo wa Shetani, njia zake mbaya sana na kuangamizwa kwake (Mwanzo 3: 1 – 7, 14 – 15). Hiyo ndiyo sababu yeye anavishambulia. Anachukia kufichuliwa, na katika vitabu hivyo anafichuliwa vile yeye alivyo hasa. Yesu alisema juu ya Shetani, "Yeye hana sehemu ndani yangu na Mimi sina sehemu ndani yake." Shetani angetaka kuthibitisha jambo hilo vinginevyo; lakini hawezi, kwa hiyo yeye hufanya yote awezayo kuondoa imani katika Neno. Lakini wakati Kanisa litakapokataa kumwamini shetani na liamini ufunuo wa Roho wa Neno, milango ya kuzimu haiwezi kulishinda.

Hebu tu niingize neno hapa kutoka katika huduma yangu mwenyewe, kama hamtajali. Nyote mnajua ya kwamba karama hii maishani mwangu ni ya kiroho. Ni karama ambapo Roho Mtakatifu anaweza kutambua magonjwa, na mawazo ya mioyo ya wanadamu, na mambo mengine yaliyojificha ambayo ni Mungu tu angeweza kujua na halafu anifunulie mimi. Laiti mngaliweza kusimama pamoja nami na muone nyuso za watu wakati Shetani anapojua atafichuliwa. Sasa, mimi sineni habari za watu. Ni kwamba Shetani ameyashikilia maisha yao kwa dhambi, kutojali, na maradhi. Lakini laiti ungaliziona nyuso zao. Shetani anajua atafichuliwa, na mabadiliko ya ajabu sana huja kwenye nyuso za watu. Shetani anaogopa. Anajua ya kwamba roho wa Mungu anataka kuwajulisha watu kuhusu kazi zake. Hiyo ndiyo sababu yeye anaichukia mikutano hii sana. Wakati majina yanapoitwa na magonjwa kufichuliwa, Shetani anachukia jambo hilo. Sasa hiki ni kitu gani? Si kusoma mawazo, si kuwasiliana mawazo, wala si uchawi. NI UFUNUO kwa roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo tu ninavyoweza kujua jambo hilo. Bila shaka nia ya mtu wa kimwili italiita cho chote kile ila Roho Mtakatifu.

Hebu niwaonyeshe sababu nyingine kwa nini Shetani anachukia Kitabu hiki cha Ufunuo wa Yesu Kristo Kanisani. Yeye anajua kuwa Yesu Kristo ni yeye yule jana na leo, na hata milele, Naye habadiliki. Yeye anayajua hayo mno zaidi kuliko wanavyojua asilimia tisini ya wanatheolojia. Yeye anajua ya kwamba kwa kuwa

Mungu habadiliki katika asili yake, basi vivyo hivyo Yeye habadiliki katika njia zake. Hivyo basi Shetani anajua kwa hakika ya kwamba lile Kanisa la asili pale Pentekoste lenye nguvu za Mungu (Marko 16 katika matendo) ndilo Kanisa Halisi ambalo Yesu anadai kama lake (Matendo 2: 1 – 13). Mengine yote ni ya uongo. Haina budi kuwa hivyo.

Sasa kumbukeni jambo hili. Kristo katika Kanisa la kweli ni kuendelezwa kwa Kitabu cha matendo. Lakini Kitabu cha Ufunuo kinaonyesha vile roho ya mpinga Kristo ingeingia kwenye Kanisa na kulichafua, kulifanya vuguvugu, la kawaida na lisilo na nguvu. Kinamfichua Shetani,

kikizifunua kazi zake (za kujaribu kuwaangamiza watu wa Mungu na kulipuuza Neno la Mungu) moja kwa moja mpaka wakati atakapotupwa katika ziwa la moto. Yeye anapinga jambo hilo. Hawezi kulivumilia. Anajua ya kwamba kama watu wakipata UFUNUO WA KWELI wa KANISA LA KWELI na kile lilicho, msimamo wake ni nini na ya kwamba LINAWEZA KUTENDA ZILE KAZI KUBWA ZAIDI, hilo litakuwa jeshi lisiloweza kushindwa (Yohana 14:12). Kama wao wakipata ufunuo wa kweli wa zile roho mbili katika kanisa la Kikristo, na kwa Roho wa Mungu waitambue na kuipinga roho ya mpinga-Kristo, Shetani hatakuwa na nguvu mbele zake. Yeye kwa dhahiri atashindwa leo hii kama vile wakati ambapo Kristo alimpinga kwa kila jitihada yake ya kumshinda Yeye huko nyikani. Naam, Shetani anachukia ufunuo. Lakini sisi tunaupenda. Tukiwa na ufunuo wa kweli maishani mwetu, milango ya kuzimu haiwezi kutushinda, bali tutaishinda.

Mtakumbuka ya kwamba nilitamka hapo mwanzoni mwa ujumbe huu ya kwamba Kitabu hiki tunachosoma ni ufunuo halisi wa Yesu, Mwenyewe, katika Kanisa na kazi yake katika nyakati zijazo. Halafu nikasema ya kwamba inahitaji Roho Mtakatifu kutupa ufunuo la sivyo tutashindwa kuupata. Tukiyaunganisha mawazo haya mawili pamoja mtaona kwamba haitachukua tu masomo tu ya kawaida na akili kukifanya Kitabu hiki halisi. Itahitaji nguvu za Roho Mtakatifu. Hiyo inamaanisha Kitabu hiki hakiwezi kufunuliwa kwa mtu yeyote isipokuwa kwa kundi maalum la watu . Itahitaji mtu aliye na ono la kinabii. Itahitaji uwezo wa kusikia kutoka kwa Mungu. Itahitaji mafundisho ya kimbinguni, si eti tu mwanafunzi alinganishaye aya na aya, ingawa jambo hilo ni zuri. Lakini fumbo linahitaji mafundisho ya Roho la sivyo halitakuwa dhahiri hata kidogo. Jinsi gani tunavyohitaji kusikia kutoka kwa Mungu na kujiweka wazi na kujisalimisha kwa Roho ili tusikie na tujue.

Kama vile nilivyokwisha kusema, Kitabu hiki (ufunuo) ndicho ukamilifu wa Maandiko. Hata kimewekwa panapofaa kabisa katika vitabu vya maandiko, mwisho. Sasa unaweza kujua kwa nini hasa kinasema ya kwamba mtu ye yote anayekisoma ama hata kukisikia amebarikiwa. Ufunuo wa Mungu ndio ambao utakupa mamlaka juu ya ibilisi. Nawe unaweza kuona ni kwa nini wao ambao wangeongeza ama kuondoa kutoka kwake wangelaaniwa. Haina budi kuwa hivyo, kwa sababu ni nani anayeweza kuongeza ama kuondoa kutoka katika ufunuo mkamilifu wa Mungu na amshinde adui? Ni rahisi namna hiyo. Hakuna kitu kilicho na nguvu za ushindi namna hiyo kama ufunuo wa neno. [1]

Unaona, kama nilivyosema katika ujumbe wangu asubuhi ya leo, tunawoga sana, kwamba tunahitaji mtu kama Sauli atufundishe sisi. Tunataka mtu kama sauli kutoka Seminari fulani atueleze sisi ni kwa jinsi gani tunapaswa kufanya dini yetu, na namna ya kulifanya hilo. Hayo ni ya upande ule mwingine wa Yordani, upande huu, Roho mtakatifu anaongoza. Juu hapa uko nje ya matope hayo. Juu hapa

hujali yale wanayowaza, Hapa juu umekufa, na maisha yako yamefichwa pamoja na Kristo ndani ya Mungu na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu (Kolosai 3:1 – 3). Hujali wewe, wewe unaishi kanaan. Unaweza kuendelea kula mahindi. Wewe ni kiumbe kipya ndani ya Yesu Kristo (2kor. 5:17). Umeshikiliwa ufike nchi ya Ahadi.

Ndugu Branham anaendelea: Nakumbuka nilisimama ng'ambo kule kama miaka thelethini iliyopita. Kabla hili jengo halijajengwa bado, ilikuwa mkutano mdogo wa hema ukifanyika hapa kwenye kona, mkutano wangu wa kwanza. Nilikuwa ninahubiri Injili hii hii, kitu hikihiki, utajiri usiochunguzika wa Kristo, ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo, kuamini kila neno kuwa ni kweli, ubatizo wa Roho Mtakatifu, uponyaji wa kiungu, Nguvu za Mungu kama vile tu ninavyohubiri leo. Hata hautofautiani kwa inchi moja nao. Mungu amezidi kunifunulia mengi ya hayo, hivyo kadiri anavyofunua, ninazidi kuwaletea (watu) hayo. Kamwe haondoi kile kilichokuwepo. Anaendelea kuongeza zaidi juu ya hayo [2].

Lakini siri hii yote inafunuliwa tu alivyo muahidi Bibi arusi wake. Kuzimu huko kinyume na ufunuo wa hii kweli, ya ufunuo wa siri hii. Lakini Bibi arusi ana simama juu yake. Huo ndio msimamo wake.
Kanisa, kwa nini unasikia njaa? Kwa nini unaona kiu? Ni Baba akijaribu kukufunulia siri hii iliyofichwa. Lakini unaruhusu mambo mengi kuiondoa hiyo njaa kutoka ndani yako. Umeruhusu kazi yako, umeruhusu mke wako umemruhusu mume wako, umewaruhusu watoto wako, umeyaruhusu masumbufu ya ulimwengu, umemruhusu mchungaji fulani, umemruhusu mtu fulani aiondoe kutoka kwako. Hali ukijua ndani moyoni mwako mnakiu, njaa. Ni Mungu anajaribu kukufunulia siri yake (unaona?) ule ufunuo. Siku ya mwisho ipo hapa. [3]

## Nukuu

[1] Nyakati saba za Kanisa Uk. 3 - 6 [2] Kufanywa wana sehemu ya 1 Uk. 117 – 118 (kiingereza) [3] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa Uk. 72 – 73.

---

Jiwe la kiroho la kujengea no. 149 kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69, – D – 75328 Schomberg, Germany simu (+49) 7235 7613, Fax (+49)– 3306)

---

Atakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia zile mbegu zitaingizwa katika magazeti na vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu iliyoteuliwa kimbele imesikia hilo (Ndg. Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho Uk. 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*